# WIKI YA ASASI ZA KIRAIA 2018

**Tarehe:** 22-26 Oktoba 2018
**Mahali:** Dodoma, Tanzania

FOUNDATION for Civil Society

## MAELEZO KUHUSU WIKI YA ASASI ZA KIRAIA 2018

KAULIMBIU: **TANZANIA YA VIWANDA: WATU, SERA NA UTEKELEZAJI**

### 1.0 Utangulizi

Asasi za Kiraia (AZAKI) zilianzishwa hapa nchini katika miaka ya 1990. Zikiwemo Asasi rasmi na zisizo rasmi. Asasi za kiraia ni pamoja na Asasi zisizo za kiserikali, Asasi zisizozalisha faida, Asasi za kijamii taasisi za kidini; vyama mbalimbali ikiwemo, vyama vya wafanyakazi, taasisi za kitaaluma na vyombo vya habari. Kwa miaka yote hii, Asasi zimekuwa zikitoa mchango muhimu katika utetezi wa haki za kijamii, utoaji wa huduma na maendeleo ya nchi kwa ujumla. Mafanikio haya yametokana na kuimarika kwa uhusiano baina ya Asasi za jamii pamoja na vyombo vya maamuzi kama Bunge na Serikali ikiwemo serikali kuu na serikali za mitaa.

Taasisi ya Foundation for Civil Society kwa kushirikiana na washirika na wadau wa maendeleo katika sekta ya Asasi za Kiraia nchini wameandaa Wiki ya Asasi za Kiraia 2018. Itakayofanyika tarehe 22 hadi 26 Oktoba, 2018 jijini Dodoma. Kaulimbiu ya wiki ya Asasi za kiraia imetokana na Mpango wa Miaka mitano wa maendeleo ya Nchi (2018/17 - 2020/21 ) uliojikita kuleta mapinduzi ya kiuchumi na maendeleo ya nchi kupitia sekta ya viwanda.

Wiki ya Asasi za Kiraia ni fursa adhimu ya kufanya majadiliano kati ya asasi za kiraia, pamoja na vyombo vya maamuzi kwa lengo la kujenga mahusiano na maelewano miongoni mwa wadau mbalimbali kwa sasa na siku zijazo na hivyo kuongeza ushiriki madhubuti wa wananchi na asasi za kiraia katika masuala muhimu kwa taifa.

Kutokana na ukweli kuwa Serikali ndie mdau mkubwa wa Asasi za kiraia nchini, kupitia taasisi ya Foundation for Civil Society Asasi za Kiraia ziliona uhitaji wa kuileta serikali karibu zaidi na kuikutanisha na Asasi pamoja na wadau wengine wa maendeleo kwa kupitia wiki hii ya Asasi za Kiraia nchini. Tukio hili linakuja wakati muafaka kulingana na sera ya serikali ya kuimarisha uchumi wa viwanda pamoja na azma ya kuhamia Dodoma

Lengo kuu la Wiki ya Asasi za kiraia ni kutoa nafasi kwa Asasi na Taasisi mbalimbali kufanya maonesha ya shughuli na huduma wanazotoa kwa jamii, sambamba na kuwezesha ushiriki wa jamii na umma wa watanzania katika ujenzi wa uchumi wa viwanda.

Kupitia wiki hii ya Asasi za kiraia, wadau wa maendeleo wamedhamiria kuungana na Serikali kutekeleza Azma ya kuelekea uchumi wa viwanda kwa kuzingatia haki, ushiriki pamoja na ujumuishi wa makundi yote katika jamii. Aidha wiki ya Asasi za Kiraia inatoa fursa ya kujifunza na kubadilishana uzoefu miongoni mwa wanajamii na wadau wa maendeleo ikiwa ndio nguzo kuu ya maendeleo endelevu. Sambamba na hili, Wiki ya asasi za Kiraia pia ni jukwaa la majadiliano na maridhiano miongoni wa wadau wa maendeleo na vyombo vya maamuzi ikiwemo serikali na Bunge. kwa lengo la kuimarisha mshikamano katika kuleta maendeleo kwa wananchi wa Tanzania. Ni fursa ya kuhabarisha umma wa watanzania kuhusu kazi na mchango wa Asasi za kiraia katika jitihada za serikali za kuleta maendeleo nchini.

## 2.0 Malengo ya Wiki ya Asasi za Kiraia

Wiki ya ya Asasi za Kiraia itafanyika Dodoma kuanzia tarehe 22 hadi 26 Oktoba, mwaka 2018. Wiki hii itazileta pamoja Asasi na Taasisi zaidi ya 300 kutoka Tanzania bara na Visiwani. Yafuatayo ni malengo ya Wiki ya Asasi za Kiraia:-

**Malengo:**

- Kuimarisha mshikamano na ushirikiano miongoni mwa wadau wa maendeleo ikiwemo serikali, bunge na Asasi za kiraia.
- Kubaini na kutumia fursa za kupashana habari, kubadilishana uzoefu na kujifunza kwa lengo la kuimarisha ushirikiano baina ya serikali, Bunge pamoja na wadau wa maendeleo.
- Kuonesha na kuzitangaza kazi na huduma zinazotolewa na Asasi za kiraia na wadau wa maendeleo, sambamba na kuhabarisha umma kuhusu mchango wao katika ujenzi wa uchumi wa viwanda.
- Kubaini mbinu na mikakati ya pamoja miongoni mwa sekta 3 muhimu katika maendeleo ya nchini ikiwemo Sekta ya Umma, Sekta binafsi na Sekta ya Asasi za Kiraia katika kutekeleza azma ya ujenzi wa uchumi wa viwanda.
- Kuimarisha mshikamano miongoni mwa mashirika yasiyo ya kiserikali, mashirika ya kijamii, Mashirika ya kidini, vyama vya ushirika na vyama vya hiari, taasisi za kitaaluma na wanazuoni pamoja na Mashirika ya kimataifa.

## 3.0 Yafuatayo ni matokeo yanayotarajiwa kupatikana katika wiki ya Asasi za Kiraia nchini:

- Kuimarika kwa ushiriki wa Asasi katika masuala ya kisera kwa kujiamini zaidi na kwa kushirikiana na Vyombo vya serikali pamoja na Bunge katika misingi ya kuaminiana.
- Kuongezeka kwa kushirikishana taarifa na upashanaji habari miongoni mwa wadau wa maendeleo.
- Jamii ya watanzania kufahamu kwa kina kazi na huduma zitolewazo na Asasi za kiraia na wadau wa maendeleo, sambamba na mchango wao katika ujenzi wa Taifa.
- Kuongezeka kwa umoja na mshikamano miongoni mwa wadau wa maendeleo. Ikiwemo mshikamano kati ya Asasi za kitaifa na za ngazi ya jamii/mashinani, Asasi za wazawa na Mashirika ya Kimataifa, wakala wa sekta binafsi pamoja na taasisi za serikali na vyombo vya maamuzi.

## 4.0 Muundo wa Wiki ya AZAKI

Wiki ya Asasi za Kiraia itajumuisha matukio mbalimbali miongoni mwa hizo ni warsha na makongamano ya kujifunza na kubadilishana uzoefu, majadiliano, maonesho n.k

a) **Sherehe za uzinduzi pamoja na kufunga wiki**: Shughuli hizi zitaashiria ufunguzi na ufungaji wa wiki ya AZAKI na kuleta hamasa kwa washiriki na wadau mbali mbali.
b) **Warsha mbalimbali:** Warsha hizi zitafanyika wakati wote wa wiki nzima kupitia mikutano yenye mada mbalimbali zitakazochaguliwa. Kaulimbiu ya Wiki ni: **Tanzania ya Viwanda: Watu, Sera na Utekelezaji**
c) **Maonesho:** Washiriki watapata fursa ya kuonesha na kutangaza kazi zao. Ushiriki katika maonesho utategemea jinsi asasi zitavyothibitisha kushiriki na kuchangia gharama za maandalizi pamoja na ununuzi wa vitendea kazi vya maonesho
d) **Utoaji huduma kwa Wananchi:** Wananchi watanufaika na baadhi ya huduma zinazotolewa na Asasi mathalani Huduma za kupima Afya, HIV/AIDS, kansa ya matiti, upimaji macho, BP, Kisukari pamoja na utoaji wa ushauri nasaha na nasihi.
e) **Burudani:** Mahusiano na maelewano hujengeka kwa vikao rasmi na visivyo rasmi. Wiki hii pia itakuwa ni fursa kwa AZAKI kujenga mitandano na mahusiano miongoni mwao na Wabunge na serikali kupitia matamasha ya michezo , vinywaji na chakula cha pamoja.

5.0 **Fursa zitakazopatikana wakati wa Wiki ya Asasi za kiraia**

Wiki ya Asasi inatoa fursa adhimu kwa Asasi za kiraia kama ifuatavyo:-:

- Kuwezesha na kugharamia warsha na makongamano ya siku nzima au nusu siku. Ikiwemo kuandaa na kuwasilisha mada, kuendesha majadiliano, kutafuta watoa mada n.k
- Kudhamini matamasha ya michezo na burudani
- Kugharamia wadau wa Asasi kushiriki katika Wiki ya Asasi na katika maonesho
- Kuratibu uendeshaji wa mada kuu na mada zinazohusu sekta mbalimbali
- Kushiriki katika kutoa mada au kuendesha mijadala
- Kushiriki katika maonesho
- Kushiriki katika maandalizi ya wiki ya Asasi kwa kusambaza taarifa na machapisho kwa wadau.
- Kushirikiana na kamati ya maandalizi katika maandalizi na uratibu wa shughuli nzima
- Fursa za kudhamini (kutoa mchango wa fedha) wiki ya Asasi za kiraia ziko katika makundi matatu (3); **Gold**, **Platinum** na **Bronze**. Tafadhali wasiliana na Foundation for Civil Society kwa maelezo zaidi.

6.0 **Umuhimu wa Wiki ya Asasi za kiraia kwa Asasi yako**

Kamati ya maandalizi inatoa ushauri kwa Asasi kushiriki kikamilifu katika wiki hii kwa sababu kuu tano (5):-

- Wiki ya Asasi za Kiraia itawezesha Asasi yako kujulikana ziaidi na wadau
- Kupandisha hadhi ya Asasi na wakurugenzi wake
- Kuwapa walengwa na wadau wako hamasa na ufahamu zaidi kuhusu Asasi yako.
- Kutengeneza urafiki na ukaribu na watu wa kada za juu serikalini, ndani ya bunge, wahisani pamoja na wadau muhimu wa maendeleo
- Kuboresha mijadala ya kisekta inayogusa Asasi yako kwa ajili ya kuongeza mshikamano na ushirikiano.

---

**Tafadhali wasilisha Fomu ya usajili iliyokamili kabla ya Tarehe 05 Oktoba, 2018.**

**Kwa mawasiliano zaidi: Barua Pepe: csoweek2018@thefoundation-tz.org / Tovuti: www.thefoundation.or.tz**
**Simu / WhatsApp: +255 762 767 237 / Instagram: csoweek2018 / Twitter: @FCSTZ / Facebook: FCSTZ**